## MBEGU BORA ZA UFUTA

### 1.0 Utangulizi

Mbegu bora za ufuta zina sifa ya kuzaa vizuri kwa tija, kuvumilia mashambulizi ya wadudu na magonjwa na hutoa mafuta mengi baada ya kuchakatwa. Mbegu bora zinatofautiana katika tabia kama vile rangi ya mbegu, muda wa kukomaa, idadi ya matawi nakadhalika. Tangu miaka ya 1990 kuna aina sita za mbegu bora za ufuta ambazo zimekwisha sajiliwa kitaifa na kimataifa na tayari zinaendelea kusambazwa kwa wakulima. Mbegu bora za ufuta zinapatikana TARI - Naliendele na maduka ya pembejeo za kilimo.

### 2.0 Mbegu bora za ufuta na sifa zake

### LINDI - 2002

Hii aina inajulikana kwa jina la Lindi sifuri mbili (Lindi-02). Mbegu zake ni nyeupe sana, hukomaa kati ya siku 100 hadi 110 tangu kupanda. Vitumba (capsule) vyake ni virefu na kila mche wa Lindi-02 huwa na mchanganyiko wa vitumba vyenye migongo 4-8. Lindi-02 hutoa mavuno wastani wa kilo 600 kwa ekari na huvumilia ugonjwa wa madoa ya majani. Mbegu za Lindi-02 zina mafuta 55%.



*Mbegu bora aina ya Lindi-02*



*Vitumba vya Lindi-02*

### NALIENDELE - 1992

Mbegu hii inajulikana kwa jina la Naliendele 92. Mbegu zake ni nyeupe na hukomaa kati ya siku 105 hadi 110. Vitumba(capsule) vyake ni virefu kama vya Lindi-02 tofauti yake ni kila kitumba huwa na migongo 4 tu na hupinda kidogo. Naliendele-92 hutoa mavuno wastani wa kilo 480 kwa ekari na huvumilia ugonjwa wa madoa ya majani. Mbegu zake zina mafuta 52%.



*Mbegu bora aina ya Naliendele-92*



*Vitumba vya Naliendele-92*

### ZIADA - 1994

Aina hii inajulikana kwa jina la Ziada 94 au Ziada. Mbegu zake zina weupe wa wastani na ni nene kidogo ukilinganisha na aina zingine za mbegu bora za ufuta. Aina hii hukomaa kati ya siku 120 hadi 130. Vitumba(capsule) vyake ni vifupi na kila kitumba huwa na migongo 4 tu. Ziada 94 hutoa mavuno wastani wa kilo 400 kwa ekari na huvumilia ugonjwa wa madoa ya majani na kuoza kwa shina. Mbegu zake zina mafuta mengi 58%



*Mbegu bora aina ya Ziada-94*



*Vitumba vya Ziada-94*

## MTONDO - 2013

Hii aina inajulikana kwa jina la Mtondo-13 au Mtondo. Rangi ya mbegu zake ni nyeupe. Hukomaa mapema kati ya siku 94 hadi 103. Vitumba (capsule) vyake vina urefu wa wastani, vinene na vina migongo 4 tu. Mtondo-13 hutoa mavuno wastani wa kilo 520 kwa ekari na huvumilia ugonjwa wa madoa ya majani. Mbegu zake zina mafuta asilimia 50.




*Mbegu bora aina ya Mtondo-13*



*Vitumba vya Mtondo-13*

## MTWARA - 2009

Aina hii inajulikana kwa jina la Mtwara-09 au Mtwara. Rangi ya mbegu zake ni chokoleti au kahawia. Hukomaa mapema kati ya siku 95 hadi 105. Vitumba(capsule) vyake ni vifupi na vina migongo 4 tu. Mche na vitumba vya Mtwara-09 huwa na rangi ya njano - dhahabu (golden-yellow) tofauti na aina zingine za mbegu bora. Mtwara-09 hutoa mavuno wastani wa kilo 600 kwa ekari na huvumilia ugonjwa wa madoa ya majani. Mbegu zake zina mafuta 53%.



*Mbegu bora aina ya Mtwara-09*



*Vitumba vya Mtwara-09*

TARI
Transforming Agriculture

# MBEGU BORA ZA UFUTA



*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509
MTWARA
Email: cdnaliendele@tari.go.tz

**Mei 2022**